

Sumu ya Risasi ni tatizo kubwa la afya lakini linaloweza kuzuiwa. Madini ya Risasi ni chuma yenye sumu kali ambayo imekuwa kutumika kawaida katika bidhaa nyingi-kama rangi, risasi ya kuchomelea, betri, shaba, radieta za gari na ufinyanzi. Risasi nyingi sana katika mwili, husababisha sumu, inaweza kusababisha matatizo makubwa ya afya na ya kudumu. Risasi kinaweza kuumiza ubongo, figo na mfumo wa neva. Hakuna kiwango cha salama cha risasi katika mwili.

Risasi ni hatari sana kwa watoto wadogo ambao wanaweza kugusana na risasi kwa njia kadhaa.

Risasi kwenye Rangi

Mavumbi yatokayo katika rangi za Risasi ndiyo chanzo kikubwa sha sumu hii. Mwaka 1978, risasi ilipigwa marufuku kutumika kwa kutengeneza rangi. Nyumba nyingi zilizojengwa kabla ya wakati huo, zinaweza kuwa na risasi. Watoto wanaweza kupatwa na sumu hii wakati wa kubomoa au matengenezo ya nyumba au sehemu za uchakavu wa rangi. Vumbi la risasi linaweza kuingia kwa njia ya pumzi au mdomoni.



Risasi kwenye udongo na Maji ya Kunywa

Udongo unaweza kuwa na risasi kutoka kwenye rangi ya risasi ambayo inabanduka nje ya majengo na kutoka kwenye moshi wa petrol yenye risasi. Risasi inaweza kuingia ndani ya maji ya kunywa kama yanapitia kwenye mabomba ya ya zamani yenye risasi, miungo yenye risasi au kuchomelea kwa risasi

Vyanzo vingine vya Risasi

Watoto wanaweza kupata sumu ya Risasi kutoka vyanzo vingine vilivyo na Risasi.

- **Risasi kwenye maeneo ya kazi au kwenye nguo za mzazi:** ujenzi na kazi za kukarabati, ukarabati wa magari na kazi za betri, kuchomelea mabomba, na kelehemu kwa kutumia Risasi.
- **Risasi kwenye sufuria na vyombo:** vyombo vilivyong'arishwa na sufuria chuma na solder risasi.
- **Risasi katika vifaa vya kihistoria, bidhaa za vitu vilivyotupwa jalalani:** samani za zamani, vifaa vya ujenzi na vitu vingine, hata kama vinaonekana kuwa safi.
- **Risasi katika Bidhaa:** vinyago na mapambo yaliyotengenezwa nchi nyingine, pipi zilizoagizwa (hususani kutoka Meksiko), vyakula vya makopo toka nchi za zingine, viungo na mchanganyiko wa viungo (hasa ikiwa huja moja kwa moja kutoka kwa nchi nyingine), funguo za chuma, marembo ya mwili na madawa ya tiba za nyumbani.
- **Risasi katika sanaa na michezo:** Vioo vilivyopakwa rangi, risasi za bunduki, visamisha ndoano na rangi za msanifu



Kuzuia sumu ya Risasi

- Kuzuia sumu ya risasi kwa watoto kwa kudumisha nyumba yako katika hali nzuri, kusafisha kwa njia salama dhidi ya risasi, na kula vyakula vyenye afya.
- Osha mikono ya watoto kabla ya kula na kulala, na safisha vinyago mara nyingi ili kuondoa vumbi lisiloonekana.
- Wape watoto vitafunio na chakula kwenye meza au wakalishe katika viti vya juu.
- Karabati rangi iliyopigwa kama inababuka au kupasuka. Weka watoto mbali na maeneo haya hadi kazi iishe.
- Tumia vitambaa vyenye unyevunyevu kusafisha sakafu. Kisha tupa vitambaa hivyo. Tumia machine ya kuvuta vumbi kulingana na chujio kwa mujibu wa sharia ya HEPA. Endesha machine katika mwendo mdogo.



- Tumia mazoea ya salama wakati wa ukarabati, kama vile kukwangua katika unyevunyevu, na usitumie msasa wa mkanda au bunduki ya moto
- Panda bustani za chakula katika udongo usiona risasi, na iwe kama hatua tatu mbali na majengo na barabara zenye magari mengi.
- Acha viatu mlangoni ili usilete ndani ya nyumba udongo ambao unaweza kuwa na risasi.
- Chunguza kiwango cha risasi ya maji yako. Agiza kifaa cha majaribio cha maji ya kunywa kwa dola 12 kwa kuita namba 800-660-9997.

Kwa taarifa zaidi juu ya madhara ya sumu ya madini ya rosado, piga simu namba: 800-439-8550 au ingia mtandaoni healthvermont.gov/lead.